# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26-2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz

Mji wa Serikali, Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UTAPELI UNAOFANYWA NA BAADHI YA KAMPUNI ZA KUUZA MAGARI ZA NCHINI JAPAN

**Dodoma, 24 Septemba 2020**

Ubalozi wa Tanzania uliopo Tokyo nchini Japan umekuwa ukipokea malalamiko mengi kutoka kwa Watanzania wanaodhulumiwa fedha wakati wakijaribu kununua magari kwa njia ya mtandao. Malalamiko hayo pia yanahusisha kutotumiwa magari yao kwa wakati na kutumiwa magari ambayo hayana sifa na vigezo vilivyoainishwa kwenye mtandao.

Ubalozi kwa nyakati tofauti umefuatilia kwa karibu suala hili kwenye Mamlaka husika za Japan na unatoa ushauri ufuatao ili kuepuka matatizo hayo yasijitokeze tena:-

- Fanya uchunguzi wa kina kabla ya kutuma fedha kwa mtu ama kampuni yoyote ile; inayojihusisha na uuzaji wa magari;
- Kabla ya kuagiza gari ni vyema kuangalia tovuti zaidi ya moja ili uweze kulinganisha bei na kufahamu bei ya wastani ya gari husika, kampuni inayouza gari kwa bei ya chini sana kuliko nyingine lazima itiliwe mashaka;
- Inashauriwa utume baruapepe kwa Taasisi iliyosajiliwa na kutambulika na Serikali ya Japan (Japan Used Motor Vehicle Exporters Association–JUMVEA); ili wakusaidie kufanya uhakiki wa Kampuni husika. Wanaweza kuhakiki Kampuni yoyote hata kama si mwanachama wao. Huduma hii hutolewa bure.
- Ukiwa na mashaka nunua gari kupitia kampuni ambayo ni mwanachama wa JUMVEA. Kuna Kampuni zaidi ya 250 ambazo ni mwanachama wa JUMVEA na wanatumia mfumo maalum wa malipo JUMVEA SAFE TRADE (JUST) ambayo inamlinda mteja. Kwa maelezo zaidi tembelea Tovuti yao https://jumvea.or.jp ama tumia kampuni za kijapan zenye matawi nchini na kutambulika kwa mujibu wa sheria za Tanzania;
- Ikumbukwe kuwa, fedha ikishatumwa Japan ni vigumu sana kurejeshwa kutokana na sheria za nchi hiyo. Mamlaka za kisheria za Japan kama Polisi na Waendesha Mashtaka huanzisha shauri dhidi ya kampuni au mtu aliyekiuka mkataba kwa kutumia hupokea mikataba halali inayotambulika Japan kama nyaraka za kuanzisha shauri dhidi ya kampuni au mtu aliyekiuka mkataba na sio Ankara za Malipo ambazo wengi huwa nazo; na
- Ubalozi unawasihi watu wote kuzingatia ushauri ulitolewa hapo juu na kufuata taratibu za biashara za Kimataifa, ili waepuke kutapeliwa au kudhulumiwa. Kutuma fedha za kigeni bila kupata mali tarajiwa si tu kunaleta madhara makubwa kwa mtumaji na familia yake, bali huharibu akiba ya nchi ya fedha za kigeni bila kupata thamani tarajiwa.

Imetolewa na:

Emmanuel Buhohela
**Mkurugenzi, Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**